Jamvi la Habari Uk. 8, Tarehe 10/06/2021

Alisema kuwa kwa sasa mfuko

# Ulega atoa miezi 3 kuanza ukarabati Machinjio Dodoma

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema serikali haitomvumilia afisa yeyote ambaye ataisababishia hasara serikali kwa kushindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato.

Ulega, alisema serikali kwa sasa iko imara katika ukusanyaji wa mapato na kwamba afisa ambaye atakua mzembe kwenye kusimamia ukusanyaji huo ataondolewa mara moja na kwamba hatovumiliwa afisa yeyote atakayeshindwa kutekeleza wajibu wake.

Naibu Waziri Ulega alitoa kauli hiyo wakati alipofanya ziara ya kutembelea Machinjio ya Dodoma ambapo ametoa miezi mitatu kwa uongozi wa machinjio hiyo kuboresha miundombinu ili iweze kutoa huduma na kuchangia ipasavyo pato la Taifa.

"Sijaridhishwa na Miundombinu ya machinjio yetu hii ambayo ni miongoni mwa machinjio bora sana, hivyo natoa miezi mitatu kwenu uongozi ya kufanya maboresho na ninataka ndani ya wiki moja muwe mshaanza maboresho hayo na mimi kila mwezi nitakua nakuja kukagua.

"Lengo letu Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona machinjio yetu inafanya Kazi katika ubora unaotakiwa, na kama mlivyoona Rais wetu alikutana na wawakilishi wa falme za kiarabu ambapo ndipo pia tunauza nyama kwa wingi, hivyo na sisi hapa inatupasa tubadilike," alisema Ulega.

Ulega, alisema ukusanyaji wa mapato ya serikali uende sambamba na uboreshaji wa mazingira mazuri ya biashara ili kumfanya anaelipa ushuru aone ni haki kulipa na kwa kufanya hivyo biashara ya mifugo itakua zaidi.

Kwa upande wake Meneja wa Machinjio hiyo, Mwita Victor, alimuahidi Naibu Waziri kuwa watayatekeleza maagizo yake katika muda aliotoa jli kutochangia kudorora kwa biashara hiyo.

"Tunaahidi kutekeleza maagizo yako katika muda uliotupangia na kwa kuanza tunaanza na ubanaji wa matumizi ili tuweze kutumia mapato vizuri katika kufanya maboresho ya Miundombinu na mazingira kwenye machinjio yetu," alisema Mwita.

Scanned with CamScanner

## Ruvuma kupandisha hadhi hifadhi mbili za misitu

Na Stephano Mango, Ruvuma

MKOA wa Ruvuma umeridhia kupandisha hadhi hifadhi mbili za misitu kuwa mapori ya akiba kwa lengo la kuboresha Sekta ya Utalii Kusini.

Mshauri wa Maliasili na Utalii Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe aliyataja mapori hayo kuwa ni Gesimasowa lenye ukubwa wa kilomita za mraba 764, lililopo Halmashauri ya Madaba wilayani Songea na pori la Litumbandyosi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 494 lililopo wilayani Mbinga.

"Mapori hayo ni sehemu ya

# Mtaka ataka ranchi ya mifugo Kongwa kunufaisha wafugaji

Na Zena Mohamed, Dodoma

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka ameahidi kukutana na uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kujadili namna ya kuwawezesha Wafugaji mkoani hapa, kunufaika na Shamba la Mifugo la Serikali lililopo wilayani Kongwa (Kongwa Ranch).

Mtaka aliyasema hayo jijini hapa juzi wakati akifungua mkutano wa wafugaji wa Mkoa wa Dodoma ambapo alisema, atazungumza na Wizara ya Mifugo ili kuwapatia wakulima wa hao vitalu vya ardhi kwenye shamba hilo la mifugo, lenye ukubwa wa hekta 38,000 sawa na ekari 95,000 kwa utaratibu wa kukodisha ili wakulima hao waweze kupata maeneo ya kutosha ya kuendeshea shughuli za ufugaji wa kisasa na uoteshaji malisho ya mifugo.

"Kipaumbele changu katika Sekta ya Ufugaji kwenye Mkoa wa Dodoma ni kuendesha ufugaji bora, wa kisasa, wenye tija na uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya mifugo nyama, maziwa, ngozi, pembe na kwato.

"Dodoma ya zamani soko lake lilikuwa mndani, lakini unayoiendea sasa ni Dodoma ya viwanda ya machinjioni, anza kujiandaa, mlikotoka ng'ombe ilikuwa shughuli ya kimaskini wanashinda juani na wewe unashinda juani unakoendea kwenye ufugaji wa kisasa, fuga vizuri nenepesha ng'ombe na kuza soko," alisema.

Awali Katibu wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Dodoma, Reginald Lubeleje alisoma risala kwa Mkuu wa Mkoa ambapo wamemlalamikia kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maeneo ya kufugia ya maeneo ya malisho kwani maeneo mengi yaliyopo yana changamoto ya migogoro ya mipaka, ukosefu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, ukosefu wa huduma muhimu kama maji na majosho ya kuogeshea mifugo.

Lubeleje alisema, baadhi ya maeneo ya ufugaji na malisho yamekuwa yakivamiwa kwa shughuli za kilimo kwani wakulima bado wana ukosefu wa elimu ya kutosha ya ufugaji bora na kuongeza kuwa Dodoma, lipo shamba kubwa la mifugo la serikali wilayani Kongwa (Kongwa Ranch) lakini halina mchango katika kuwasaidia wakulima na kubadili aina ya ufugaji wao kuwa ufugaji bora na wa kisasa.

Scanned with CamScanner

# Ulega: Serikali haitamvumilia atakayesababisha hasara

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema serikali haitamvumilia ofisa yeyote ambaye ataisababishia hasara, serikali kwa kushindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato.

Amesema serikali kwa sasa iko imara katika ukusanyaji wa mapato na kwamba ofisa, ambaye atakua mzembe kwenye kusimamia ukusanyaji huo ataondolewa mara moja na kwamba hatovumiliwa ofisa yeyote atakayeshindwa kutekeleza wajibu wake.

Naibu Waziri Ulega alitoa kauli hiyo wakati alipofanya ziara ya kutembelea Machinjio ya Dodoma, ambapo alitoa miezi mitatu kwa uongozi wa machinjio hiyo kuboresha miundombinu ili iweze kutoa huduma na kuchangia ipasavyo pato la taifa.

"Sijaridhishwa na miundombinu ya machinjio yetu hii, ambayo ni miongoni mwa machinjio bora sana, hivyo natoa miezi mitatu kwenu uongozi ya kufanya maboresho na ninataka ndani ya wiki moja, muwe mmeshaanza maboresho hayo na mimi kila mwezi nitakua nakuja kukagua.

"Lengo letu serikali chini ya Rais, Samia Suluhu Hassan ni kuona machinjio yetu inafanya kazi katika ubora unaotakiwa na kama mlivyoona, rais wetu alikutana na wawakilishi wa Falme za Kiarabu ambako ndipo pia tunauza nyama kwa wingi, hivyo na sisi hapa inatupasa tubadilike," alisema.

Ulega alisema ukusanyaji wa mapato ya serikali, uende sambamba na uboreshaji wa mazingira mazuri ya biashara ili kumfanya anayelipa ushuru aone ni haki kulipa na kwa kufanya hivyo biashara ya mifugo itakua zaidi.

Kwa upande wake Meneja wa machinjio hiyo, Mwita Victor alimuahidi Naibu Waziri kuwa watayatekeleza maagizo yake katika muda aliotoa ili kutochangia kudorora kwa biashara hiyo..

"Tunaahidi kutekeleza maagizo yako katika muda uliotupangia na kwa kuanza, tunaanza na ubanaji wa matumizi ili tuweze kutumia mapato vizuri kwenye kufanya maboresho ya miundombinu na mazingira kwenye machinjio yetu," alisema.

Majira Uk. 17, Tarehe 10/06/2021

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.10, Tarehe 10/06/2021



Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, akijibu baadhi ya maswali Bungeni Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Scanned with CamScanner